



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



---

TAARIFA KWA UMMA


KUHUSU WANAFUNZI 1,815 KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE 2023

Tunduma, Tarehe 12 NOVEMBA 2023

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Tunduma, Philemon Magesa anapenda kuutaarifu umma kuwa jumla ya **Watahiniwa 1,815** wa Kidato cha Nne katika Halmashauri hiyo, wanaungana na wenzao nchini kufanya **Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne mwaka 2023** ambao unafanyika kuanzia **Jumatatu tarehe 13 Novemba 2023** utamalizika **Alhamisi tarehe 30 Novemba 2023**.

Kati ya Watahiniwa hao **1,815**, **Wavulana ni 787** na **Wasichana ni 1,028** ambapo Watahiniwa wa Shule ni **1,718 (Wavulana ni 754 na Wasichana ni 964)**, Watahiniwa wa Kujitegemea ni **97 (Wavulana ni 33 na Wasichana ni 64)** na Watahiniwa wa Mtihani wa Maarifa (QT) ni **118 (Wavulana ni 54 na Wasichana ni 54)** ambapo vituo vya kufanyia mitihani ni **17**.

Baraza la Madiwani, Menejimenti na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Tunduma inawatakia kheri Watahiniwa wote wa Kidato cha Nne mwaka 2023 katika Mtihani wao wa kumaliza elimu ya Sekondari na kuwaomba kwa Mwenyezi Mungu ili wafanye vema na huku wakizingatia taratibu zote za Mtihani wa Taifa.

  
Benton J. Nollo

**Mkuu Wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Mji Tunduma**